10/11/2025

# TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

## HOSPITALI YA WASSO – JIMBO KUU KATOLIKI ARUSHA

## WILAYA YA NGORONGORO

Hospitali ya Wasso ni hospitali ya kanisa jimbo kuu katoliki la Arusha inayotoa huduma za afya kwa jamii ya Ngorongoro na maeneo ya jirani.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wasso anakaribisha maombi ya kazi kwa kada ya **Mpishi wa Hostel ya wageni** na **Mhandishi wa vifaa Tiba (Bio-Engineer)** wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zilizo wazi kama ifuatavyo;

**1. MPISHI DARAJA LA II (COOK GRADE II)** NAFASI (1)

**a) SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na cheti cha kidato cha nne au kidato cha sita.
- Awe na Cheti cha Hotel Management kutoka chuo kinachotambulika na Serikali.
- Awe na uzoefu wa angalau miaka **miwili (2)** katika Hoteli, Lodge au hosteli ya kitalii.
- Uwezo wa kuandaa vyakula vya kimataifa (Continental & African dishes) utapewa kipaumbele.
- Awe na uelewa wa masuala ya **usafi wa chakula, huduma kwa wateja (Customer care), na usalama wa chakula (Food safety standards).**

  Awe na maadili mazuri, Mwaminifu, mchapakazi, na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu kulingana na ratiba ya wageni.

**b) MAJUKUMU YA KAZI**

- Kupika na kuandaa chakula bora kwa wageni na watalii wanaofikia katika Hospitali yetu kwa kuzingatia viwango vyenye ubora.
- Kuandaa menyu mbalimbali (Local & continental dishes) kulingana na mahitaji ya wageni.
- Kuhakikisha sehemu ya jikoni, vyombo na vifaa vya upishi vinakuwa safi muda wote.

- Kusimamia upokeaji, uhifadhi na matumizi sahihi ya malighafi za chakula.
- Kuhakikisha huduma za chakula zinatolewa kwa wakati, kwa usafi na kwa ukarimu.
- Kushirikiana na Uongozi katika kuboresha huduma na kuridhisha wateja.
- Kuhakikisha gharama za upishi zinadhibitiwa na kuzingatia bajeti ya mapato ya hostel.